**LEARNING BY EAR 2012**

# “Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono”

## EPISODE 10: ‘Hii ni hadithi yangu’

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREAD: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE:   PATO JOINED BY BOMBA WHILE RUNNING**

- **Pato (f, 16)**
- **Bomba (m, 18)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: NURU AND JUDY IN A COUNSELLING SESSION**

- **Judy (f, 40)**
- **Nuru (f, 30)**
- **Pato (f, 16)**
- **Dulu (m, 40)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## SCENE THREE: SEXUAL VIOLENCE CONFERENCE

- **Judy (f, 40)**
- **Allan (m, 10)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu katika kipindi ambacho kinatumbuiza na kukuelimisha, kipindi cha **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hiki ni kipindi cha kumi na cha mwisho, katika hadithi yetu kwa kichwa, **'Wasaliti walo karibu'.** Kipindi kilichopita, mkuu wa waasi aliyepanga ubakaji wa wanawake chungu nzima, akiwemo, Nuru, alikamatwa. Hivi punde, atapelekwa kujibu mashtaka katika Mahakama ya Kimataifa ya International Criminal Court. Mamake Pato, Serefa, aliamua kumuunga mkono binti yake kuhudhuria kongamano linalopinga dhuluma za kingono; na bwana mdogo Allan alianza kupona majeraha ya ulawiti aliyofanyiwa na babake wa kambo. Je, hadithi hii itakwisha vipi? Tega sikio kusikiliza kipindi hiki cha mwisho, kinachoitwa: **'Hii ni hadithi yangu'.** Tunaanza shuleni kwa Pato, alipoanza tena mazoezi yake ya asubuhi. Bomba, mwanafunzi mwenzake alikuwa anasubiri wakati huu kwa hamu na gamu.

**SCENE ONE: PATO JOINED BY BOMBA WHILE RUNNING**

1. **SFX: EARLY MORNING ATMO**

2. **PATO:** **(stretching and warming up)**

3. **BOMBA:** Pato, Pato…sasa..

4. **PATO:** **(screams)** Woooi…! Usinigutushe tena wakati mwengine! Unataka nini kwangu?

5. **BOMBA:** Ati nataka nini? **(chuckles)** Hilo ni swali la kijinga. Yaani wajifanya huelewi sio.

6. **PATO:** Kwa kweli sijui. Labda simu mpya, pengine.

7. **BOMBA:** **(laughs)** Unachekesha… Sikiliza, kwanini tusikimbie pamoja msituni? Najua mahala pazuri pa mazoezi…

8. **PATO:** **(cuts him short)** Hapana! Nitafanya mazoezi peke yangu. Nataka kukimbia peke yangu. Tafadhali usijaribu kunikaribia.

9. **BOMBA:** Ah tulia nawe, acha wasiwasi… siwezi kukudhuru **(steps closer)**

10. **PATO:** Usinikaribie. Ninakuonya. Tafadhali nenda au nitapiga yowee. **(screams)** La! usinishike! Husikii? Wuuuuiiiiiii.

11. **SFX: FOOTSTEPS RUNNING AWAY**

12. **PATO:** **(running away)** Nisaidieni!!!!! Jamani nisaidieni!

13. **BOMBA:** **(shocked)** Lahaula! Huyu msichana ni mwendawazimu. Kwani nimefanya nini? Nimemshika bega tu. Mbio na fujo zote za nini?

**14. MSIMULIZI:** Pato hana wazimu lakini anampa ilani Bomba kuwa hastahili kumkaribia. Pato bado anauguza jeraha la kihisia na kimawazo baada ya dhuluma alizopitia mikononi mwa mwalimu wake – Bw. Maneno. Anahitaji kueleweka kuwa sasa ana hofu na yeyote ndio sababu hakuwa na amani wakati Bomba alipomkaribia wakati ule. Yaliyomsibu kutoka kwa mwalimu wake bado yamo bongoni mwake. Judy anazidi kumsaidia Pato aweze kujizatiti zaidi, na kutoweka kwenye mazingira yasiyo salama. Na awapo kweli ana hofu, Judy alimueleza Pato aondoke mahala hapo haraka. Na ndipo akakimbia… Pato alikimbia bila kujua anakokwenda, akaipa kisogo shule yake, Bomba na punde akitahamaki, alijikuta alikuwa amesimama mbele ya mlango wa kituo cha Judy, akihema na kushangaa amefikaje pale. Kituo hicho kiko umbali wa kilomita kumi kutoka shule yao, Judy alikuwa na ushauri wa kibinafsi na Nuru.

**SCENE TWO: NURU NA JUDY USHAURINI**

**15. JUDY:** Nuru, nafurahishwa sana na kujitolea kwako katika ushauri. Wengi kama wewe hushindwa. Hio huchukuwa miaka kwa wengine, na wengine kamwe hawathubutu.

**16. NURU:** Shukran, Judy. Pongezi ni kwako. Unajua nilipokuja hapa hata nilikuwa nimekwishamua kujiangamiza. Unajua hata mume wangu Dulu aliniacha. Ushauri wako umenipa nguvu ya kupambana na maisha. Na kukutana na hawa manusura wengine, tukaweza kusaidiana – pia kumenipa nguvu. Nimeona kuwa siko peke yangu.

**17. JUDY:** Nuru, unalionaje wazo la hilo kongamano tunaloandaa? Unafikiri unaweza kueleza umma kisa chako?

**18. NURU:** Ndiyo, tayari nimekwishafanya uamuzi na nitaeleza watu mkasa wangu. Nimejiandaa kifikra, na niko tayari kuwapa nasaha wanawake wengine, wenye hali kama hii. Muhimu nataka watu wajue kisa changu.

**19. SFX: DOOR BEING OPENED**

**20. JUDY:** **(surprised)** Pato! Kuna nini? Uko sawa?

**21. PATO:** **(catching her breath)** Ndiyo… nilikimbia … kama ulivyoniambia… nimekimbia nikafika hapa. Nilihofu, na uliniambia nikimbie. . nilihisi mwanafunzi mwenzangu alitaka kunitongoza… lakini sitaki sasa…

**22. JUDY:** Usijali. Utakuwa sawa.

**23. NURU:** Haya, keti nilikuwa namalizia ushauri. Ngoja nikuletee kikombe cha maji – unaonekana umechoka…

**24. PATO:** Sawa maji yatanifaa. Asante, Nuru. Nashukuru.

**25. SFX: CHAIR BEING DRAGGED, FOOTSTEPS, DOOR OPENING**

**26. JUDY:** Sasa niambie, Pato; kumetokea nini?

**27. PATO:** Kuna kijana anaitwa Bomba… kwanza aliniambia twende naye msituni, halafu akaanza kunikaribia.. akataka kunishika… nikahisi vibaya… nikatoroka.. nikakimbia bila kujua naenda wapi ndiyo nikafika huku kituoni…

**28. JUDY:** Umefanya vyema Pato. Nafurahi umekuja.

**29. PATO:** Judy, kama nitazungumza kwenye hilo kongamano Jumamosi... unafikiri wasichana wenzangu watafaidika?

**30. JUDY:** Pato, bila shaka. Wanahitaji kujua – kama wewe hivi ulivyofanya - yanayowatokea sio makosa yao – muhimu waseme wapate kusaidika! Lakini ni uamuzi wako, hakuna atakaye kulazimisha. Ukiwa tayari kuwaeleza watu kisa chako, utaniambia.

31. **MSIMULIZI:** Wakati Pato na Judy katika chumba cha ushauri, Nuru amekwenda kumletea Pato bilauri ya maji. Hakujuwa kuwa wakati huu Dulu, mume wake, anakuja kumfuata huku kituoni. Amekuwa akimtafuta Nuru kwa wiki kadhaa sasa, aliporudi kijijini Nuru alikua ametoweka. Mwisho alikumbuka kumueleza kuhusu Judy na shirika lake… anatumai Nuru alikuja huku. Sasa, Dulu ana yapi ya kumueleza mkewe baada ya muda wote huu walioachana? Hebu tusikilize…

32. **SFX: TAP WATER RUNNING AND FILLING A GLASS**

33. **DULU:** Nuru!

34. **SFX: GLASS FALLING AND BREAKING**

35. **DULU:** Nuru, nisamehe. Sikujuwa ilikuwa nakutisha.

36. **NURU:** Unataka nini, Dulu?

37. **DULU:** Tunaweza kuketi pahala tukazungumza?

38. **NURU:** Sidhani…. sina mahala wala nafasi hiyo... Ni nini umesahau kwangu lakini? Si uliniacha! Wewe ulisema kuwa umeshindwa kuwa mume wangu, na ukataka kuishi peke yako. Si uko sawa sasa?

**39. DULU:** **(sorrowful)** Nuru, niseme nini… nilikuwa mjinga. Niliondoka kwa sababu ulikuwa umebakwa, na jamii ikanitenganisha na wewe. Wote wakatuepuka baada ya tukio lile, na nisingeweza kuishi katika hali ile… lakini imenichukua muda wote huu kujua wewe ndiye maisha yangu… sina mwengine wala chengine maishani…

**40. NURU:** Aha, kweli? Dulu - uliniacha, wakati ambao nilihitaji msaada zaidi. Nilikuhitaji, na wewe ukanitupa kama jongoo na mti wake!

**41. DULU:** Nuru, tafadhali nakuomba… tuanze maisha yetu upya. Nina uzito moyoni – tulimpoteza hata mtoto baada ya tukio lile… lakini sisi ni familia moja. Tafadhali nipe nafasi ya pili.

**42. NURU:** Sijui, Dulu… kwa kweli sielewi. Ghafla baada ya tukio lile nimekuwa na mtazamo tofauti kuhusu wanaume. Siwaamini tena wanaume. Hata wewe pia. Samahani.. lakini hivyo ndivyo ninavyohisi.

**43. DULU:** Ni sawa, naelewa… Nuru, tunaweza kupambana na haya yote tukiwa wawili. Nitakuwa mvumilivu, naapa. Nitakupa msaada wowote utakao lakini tafadhali nikubali tena maishani mwako.

**44. NURU:** Sikuwahi kukutoa maishani mwangu, ni wewe ulijitoa!

**45. DULU:** Nuru - nakuhitaji. Niko tayari kwa lolote...

**46. NURU:** Sio jambo la haraka. Usiniharakishe. Pia kuna jambo unafaa kujua. Judy ameandaa kongamano la kushinikiza serikali kutengeza sheria dhidi ya dhuluma za kingono Jumamosi hii na mimi nimejitolea kueleza mkasa wangu kwa umma.

**47. DULU:** **(proudly)** Nuru, itakuwa vyema! Kongamano hilo limetangazwa nchi nzima. Utapata fursa ya kuzungumza mbele ya watu mashuhuri – hata litapeperushwa hewani kwenye runinga! Umejiandaa kweli? Unahitaji nikusaidie kuandika hotuba hiyo?

**48. NURU:** Sitokuwa natoa hotuba, Dulu.

**49. DULU:** Ati? Unamaanisha nini, hutatoa hotuba? Utakuwa unawaeleza nini?

**50. NURU:** Nitakuwa nawaeleza kisa changu.

**51. DULU:** **(shocked)** Hapana… Nuru, huwezi! Unafikiri hilo linamaanisha nini? Nchi nzima itakuwa imejua yaliyotokea! La, Nuru! Usijiumbue kiasi hicho.

**52. NURU:** Lakini hivyo ndivyo tutakavyo. Tunataka watu wajue mikasa tuliyoipitia. Wajue tunapitia nini - kififkra, kimwili na kihisia. Watu wajue yalioko kwenye familia zetu, tunavyochukuliwa na jamii – wajue tunahisije. Kwa kufanya hivyo tu ndiyo watajua jinsi ya kusaidia na kujali. Nilijitolea kuzungumza, kwa niaba ya maelfu ya wanawake walioathirika kama mimi. Wengi hawana ujasiri wa kueleza mikasa yao.

**53. DULU:** **(resigned)** Naona umeamua na hutaki kurudi nyuma… **(sighs)** Nuru, nakuhofia… lakini kama itakuwa ndiyo amani kwako… basi niko na wewe. Nitakusaidia kwa vyovyote vile.

**54. NURU:** Asante, Dulu. Lakini sijui hatima yetu sisi wawili. Ni kama nilivyosema: nahitaji muda.

**55. NARRATOR:** Uzito na msongo wa mawazo umempungukia Dulu baada ya kumuona Nuru, na kujua anaendelea vyema. Amejua anahisi kusalitiwa: alimuacha alipomuhitaji, sasa anahitaji kujenga upya uaminifu huo. Itakuwa ngumu kwa wote wawili. Lakini wanaona wakipata muda, huenda wakawa tena familia moja. Wote wanakwenda kuongea na Judy, anayehimiza kuwa Dulu anahitaji ushauri kwa yale yaliomfika mkewe ili waweze kuishi tena pamoja. Muathiriwa anapomueleza mtu, wanahitaji umakinifu wa yule anayeelezwa, uwe na subira na wao, na usiweke mzaha kati yenu. Lakini hata hivyo, muelezwa lazima awe makini aweze kutompa aibu au haya muathiriwa. Wasiwaulize kwanini walinajisiwa, au kuwashurutisha kwa maswali. Manusura hawafai kulaumiwa kwa makosa ya ubakaji waliofanyiwa! Yote hayo yanahitaji kufunzwa Dulu.

Siku chache baadae, shirika la Judy linaandaa kongamano kupinga dhulma za kingono. Limepata uungwaji mkono kwa kiasi kikubwa sana, hususan baada ya mkuu wa waasi wa kuongoza ubakaji wa makundi kwa wanawake, kukamatwa. Watakaoalikwa ni watu wakuu serikalini, wageni mashuhuri, waandishi wa habari, na umma kwa ujumla. Judy ameachwa mdomo wazi kwa mwitikio huo na ridhaa ya umma mzima.

## SCENE THREE: SEXUAL VIOLENCE CONFERENCE

**56. SFX: ATMO OF LARGE CROWD IN HALL**

**57. JUDY:** **(testing mic)** Nawasalimu… kwa niaba ya shirika langu kwa kauli mbiu yetu kwa kingereza ni “**Stand Up to Sexual Violence**”, napenda kuwaalika nyote katika kongamano hili. Jina langu ni Judy, lakini si mimi msemaji leo hii. Wazungumzaji wote siku ya leo ni manusura wa dhuluma za kingono. Mikasa hii ni ya kuogofya na kusikitisha. Mtajionea kuwa sio wanawake pekee wanaoathirika. Mtamsikia kijana mdogo, wasichana wadogo, mke aliyebakwa na kundi la watu, na mengineyo mengi. Hii ndiyo mikasa yao, matarajio yetu ni kuwa serikali na kila mmoja wetu ataona haja ya kuweka sheria dhidi ya uovu huu. Wa kwanza kusema atakuwa kijana mdogo. Ameweka mkasa wake katika maandishi na atatusomea, karibu Allan...

**58. SFX: RESERVED APPLAUSE FOLLOWED BY CAMERA FLASHES**

**59. ALLAN:** Jina langu ni Allan. Nimefikia miaka 11 leo, na hii ndiyo hadithi yangu…

**HITIMISHO:**

Huku mmoja baada ya mwengine katika wasemaji akieleza yaliyomsibu. Kila mmoja alikuwa akiingiwa na hisia tofauti. Serikali ikaona haja ya kuweka mikakati ya kisheria na adhabu kwa waasi wa dhuluma hizi. Watu wakaanza kuona ukweli kuwa waathiriwa ni kaka zao, dada zao, wake wao, jirani zao na hata marafiki wao – hivyo wanahitaji msaada wao na kuwatia moyo. Kitengo cha afya kikakubali kuajiri wataalamu wengi kuhusiana na mikasa hii; na polisi wakahitaji kufunzwa jinsi ya kuwahudumia waathiriwa hawa. Upande wa Dulu … alikuwa kaketi katikati ya ukumbi. Nuru alipoanza kueleza kisa chake aliona ari mpya na nguvu mpya aliyokuwa nayo mkewe, akapendezwa, na akajilaumu kwa kumuacha wakati kama ule wa majaribu. Ameamua kufanya lolote ili kuonesha uaminifu wake kwa mkewe.

Na kwa hayo tunafikia hatma ya mchezo huu wetu wa redio uliokuwa unamulika masaibu ya dhuluma za kingono barani Afrika. Mchezo huu uliandikwa na Chrispin Mwakideu. Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kingine tembelea tovuti zetu dw.de/lbe.  Au mtandao wetu wa Facebook. Hadi tutakapokutana tena -  kwaheri ya kuonana.